التوبة - سواحيلي

# Toba




جمعية الدعوة بالزلفي

جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي

هاتف: ٤٢٣٤٤٦٦ ٠١٦ - فاكس: ٤٢٣٤٤٧٧ ٠١٦

# Toba

## التوبة - سواحيلي

Kimetafsiriwa na kuhakikiwa na:
Ally Nassor Ally
Abdallah Ally Chumbe
Abubakar Kassimu Abubakar
Yassir Salim

جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات في الزلفي
Tel: 966 164234466 - Fax: 966 164234477

# التوبة - سواحيلي

## أعده وترجمه للغة السواحيلية

## جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي

## الطبعة الأولى: ١٤٤٤/٠٦ هـ


ⓒ جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي ، ١٤٤٤هـ

*فهرسة مكتبة الملك فهد الوطنية أثناء النشر*

جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي
التوبة / لغة السواحلية. / جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي .- الزلفي ، ١٤٤٤هـ
٣٦ ص ؛ ..سم

ردمك: ٩٧٨-٦٠٣-٨٣٩٩-٠٢-٦

١- التوبة ٢- الوعظ و الارشاد أ.العنوان

ديوي ٢١٣ ١٤٤٤/٥٨١٢

رقم الإيداع: ١٤٤٤/٥٨١٢
ردمك: ٩٧٨-٦٠٣-٨٣٩٩-٠٢-٦

# Utangulizi

Kila Sifa Njema Anastahiki Allah, na Rehma na Amani zimfikie Mtume wake. Ama baada ya hayo:

Allah - Mtukufu- Amesema ***"Anayetenda maovu, ama kuidhulumu nafsi yake kisha akataka msamaha kwa Allah, atamkuta Allah kuwa ni Msamehevu na ni Mwenye Huruma."***

# Fadhila za Toba.

Kila Sifa Njema Anastahiki Allah na Rehma na Amani zimfikie Mtume ﷺ, na jamaa zake na Masahaba zake wote. Ama baada ya hayo:

Mtu mmoja alikuja kwa Ibrahim Ibn Ad-ham – Allah Amrehemu - akasema: 'Hakika nimeifanyia *Israfu* (kuidhulumu) nafsi yangu kwa kufanya Madhambi naomba nipe mawaidha.' Ibrahim akamjibu: 'Ukinikubalia mambo matano na ukayaweza kuyatekeleza basi maasi hayatakudhuru.' Yule mtu akauliza: 'Ni mambo gani hayo?' Ibrahim akamjibu: 'Ukitaka kumuasi Allah usile Riziki

Yake!’ Yule mtu akauliza: ‘Nitakula wapi? Wakati kila kilichomo Ardhini ni Riziki Yake?’ Ibrahim akamjibu: ‘Hivi inakuwa vizuri kula Riziki ya Allah ilihali unamuasi?’ Yule mtu akajibu: ‘Hapana!’ Akasema:

**‘Lete jambo la pili.’**

Ibrahim akasema: ‘Ukitaka kumuasi Allah usiishi kwenye Ardhi Yake.’ Yule mtu akajibu: ‘Hili ni kubwa kuliko la kwanza! Nitaishi wapi sasa?’ Ibrahim akamjibu: ‘Hivi itakuwa vizuri kula riziki ya Allah ukaishi kwenye Ardhi Yake, kisha unamuasi?’ Yule mtu akajibu: ‘Hapana!’ Akasema:

**‘Lete jambo la tatu.’**

Ibrahim akasema: ‘Ukitaka kumuasi Allah nenda sehemu ambayo yeye hatokuona.” Yule mtu akajibu: ‘Nitaenda wapi, ilihali Allah Anaona yaliyo ya siri na ya dhahiri?” Ibrahim akamuambia: ‘Hivi itakuwa vizuri kula riziki ya Allah ukaishi kwenye Ardhi Yake, na ukamuasi ilihali anakuona?’ Yule mtu akasema: ‘Hapana!’ na akasema:

**‘Lete jambo la nne.’**

Ibrahim akasema: “Akija *Malakul- Mauti* kuchukua Roho yako, mwambie: ‘Hebu niache kidogo ili nitubu na nitende mema.’ Yule mtu akamjibu: “Hawezi kunikubalia na wala kunicheleweshea muda.’ Ibrahim akamuambia: ‘Kama huwezi kujizuilia Umauti ili utubu na urejee kwa Allah, kwanini unamuasi?’ Yule mtu akasema:

**‘Lete jambo la tano.’**

Ibrahim akasema: ‘Wakikujia Malaika wa motoni kukuchukua ili wakuingize motoni, wakatalie usiende nao.’ Yule mtu akasema: ‘Hawatoniacha wala hawatonikubalia.’ Ibrahim akamuambia: ‘Kama ni hivyo mbona unataraji kuokoka sasa?’ Yule mtu akasema: ‘Yananitosha haya, ninamuomba msamaha Mola wangu Mlezi na ninatubia Kwake.”

Hakika Allah Amewaamrisha waja wake waliomuamini wote kutubia Kwake, Amesema Allah: ***“Tubieni kwa Allah nyote Enyi waumini ili mpate kufaulu.” [Al-Nuur: 31]***

Allah Akawagawa waja katika makundi mawili: Kuna wenye kutubia na wenye kuzidhulumu nafsi zao. Allah Amesema: ***“Na wale wasiotubia hakika hao ni wenye kudhulumu (nafsi zao).” [Al-Hujuraat: 11].***

Mahitaji ya mwanadamu kwenye Toba ni endelevu. Kila mwanadamu ni mwenye kukosea na wa-bora katika hao ni wale wenye kutubia, kama Mtume ﷺ alivyosema.

Hakika watu wengi wanaofanya makosa ni kwa sababu tu ya kuyadharau maasi, wakawa wanamuasi Allah usiku na mchana. Wapo wengine wanayaona maasi kuwa ni kitu kidogo sana na kuyadharau, na wala hawayafikirii. Ibn Masoud - Allah amuwie radhi - “Hakika muumini huyaona madhambi yake kama vile amekaa chini ya Jabali akiwa anaogopa ataangukiwa, na mtu muovu huyaona madhambi yake ni kama Nzi aliepita juu ya pua yake, kisha akamfukuza kwa mkono wake”.

Hakika muumini mwenye akili huwa haangalii udogo wa maasi, lakini huwa anaangalia ukubwa wa anayemuasi.

Mwanadamu alipokuwa sio mwenye kuhifadhiwa na kutenda makosa, ndio Allah – Mtukufu - akafungua mlango wa Toba na kuamrisha watu watubie, Allah - Mtukufu Anasema - ***“Sema Enyi waja wangu mliojidhulumu nafsi zenu! Msikate tamaa na Rehema za Allah, bila shaka Allah Husamehe dhambi zote, hakika yeye ni Mwingi wa Kusamehe, (na) Mwingi wa Kurehemu” [Al-zumar: 53].***

Mtume ﷺ amesema, *“Mwenye kutubia kutokana na Dhambi fulani ni sawa na mtu asiyekuwa na dhambi kabisa.”* [Ameipokea Ibn Majah].

Na sio hayo tu! Bali kila inapokuwa toba ya kweli basi Allah Huyabadilisha yale maovu ya mja kuwa mema. Allah - Mtukufu Amesema, ***“Isipokuwa atakayetubia na kuamini na akatenda mema, basi hao Atawabadilishia Allah maovu yao kuwa mema, na Allah ni Mwingi wa Kusamehe, (na) Mwingi wa Kurehemu.” [Al-furqan: 70].***

Na katika makosa makubwa ambayo huyafaanya Muislam: ni kuchelewesha Toba. Na katika watu kuna yule ambaye anatambua kosa lake na kujua uharamu wa matendo anayoyafanya, lakini anachelewesha kutubia. Ilihali mwanadamu hajui kuwa lini utamjia umauti! Kwa sababu hiyo, mwanadamu inampasa aharakishe kufanya toba kwa madhambi aliyoyafanya. Kama vile anavyohitajika alete *Istighfari* (kuomba msamaha) kwa wingi, kutokana na madhambi yake yote, anayoyajua na asiyoyajua, na anatakiwa aharakishe kuleta toba kutokana na madhambi aliyo yafanya, hata yakiwa madhambi hayo mengi kiasi gani. Inatakikana atambue mwanadamu kwamba hakuna dhambi kubwa kwake kama mtu kudai uungu (anaweza kufanya ayafanyayo Allah) hakika alisema Fir-aun kuwaambia watu wake: ***"Enyi watu wangu! Sijapata kujua kwenu muabudiwa asiekuwa mimi!"***

Pamoja na madai yake hayo, Allah - Mtukufu - alimtuma Nabii wake Mussa akamlinganie na kumuamrisha kutubia, amesema Allah - Mtukufu -

***"Nenda kwa Fir-auni hakika yeye amechupa mipaka mno katika kuasi. Ukamwambie, "Je unapendelea kuitakasa nafsi yako na upungufu na kuipamba na imani. Na nikuelekeze njia ya kumtii Mola wako upate kmcha na kumuogopa? [Al-Naziat: 17-19].***

Laiti Fir-auni angeitikia wito huo na akatubia, basi Allah Angemsamehe madhambi yake.

Kisha tambua kwa mara nyingine ya kwamba mwenye kufanya toba kwa dhambi aliyoifanya, kisha akarejea tena kufanya ile dhambi, huyu anatakiwa afanye toba kwa mara nyingine. Na aendelee kurejea kufanya toba kila atapokuwa anakariri kufanya dhambi hiyo ama nyingine, na wala asikate tamaa na Rehema ya Allah. Imesimuliwa na Anas - Allah amuwie radhi - amesema: Nimemsikia Mtume ﷺ akisema: amesema Allah - Mtukufu - *"Ewe Mwanadam! Hakika utakaponiomba na kunitaraji Mimi Nitakusamehe madhambi uliyonayo yote wala Sitojali, Ewe Mwanadam! Lau madhambi yako yatafikia umbali wa mbingu, kisha ukaniomba msamaha, Nitakusa-*

*mehe na wala sitojali, Ewe Mwanadam! Hakika wewe ukinijia mimi na makosa yenye ujazo wa Ardhi, kisha ukanijia bila kunishirikisha na chochote kile, Nitakujia na msamaha kwenye ujazo huo.'' [Imepokelewa na Imam Tirmidhiy]*.

Na katika watu wapo wanaokata tamaa na rehma za Allah, na hilo ima kwa kuwa na madhambi au maasi mengi, au inawezekana amefanya toba mara nyingi huku akiwa anarejea kufanya kosa hilo hilo, akidhania kwamba Allah Hatomsamehe. Hivyo basi, anaendelea kufanya maovu na kuacha toba na kurejea kwa Allah, hili ni katika makosa makubwa sana.

Hakika hakati tamaa na rehema za Allah isipokuwa kafiri. Allah - Mtukufu - Anasema, ***"Sema Enyi waja wangu mliojidhulumu nafsi zenu! Msikate tamaa na Rehema za Allah, bila shaka Allah Husamehe dhambi zote, hakika yeye ni Mwingi wa Kusamehe, (na) Mwingi wa Kurehemu." [Al-Zumar: 53]*** na akasema tena: ***"Hakika hawakati tamaa na Rehema za Allah isipokuwa watu Makafiri." [Yusuf: 87].***

Kuna wengine wanaacha kufanya toba kwenye baadhi ya maasi kwa kuogopa maneno ya watu, au anaogopa kama atafanya toba basi atapoteza nafasi yake (cheo) katika jamii anayoishi, au kazi anayoifanya. Anasahau kwamba atakwenda kaburini akiwa peke yake, atapelekwa kwa Mola wake mlezi na aulizwe juu ya matendo yake. Wala hatonufaishwa na fulani wala fulani katika wale waliokuwa wakimshawishi, na kumpambia maasi. Hapa sasa yatakiwa kila mwanadamu atambue kuwa atakaye acha jambo kwa ajili ya Allah basi Allah Atampa mbadala wa jambo hilo likiwa na kheri zaidi.

Kisha katika watu kuna mwenye kuendelea kufanya madhambi, akikemewa na kukatazwa, husema: "*Hakika Allah ni Mwingi wa Kusamehe na Mwingi wa Huruma."* Bila shaka huu ni ujinga na upuuzi. Lakini pia ni kupotezwa na Shetani kwa baadhi ya watu. Kwani Rehema za Allah ni kwa ajili ya watu wema tu na wala sio watu waovu wenye kung'ang'ania madhambi. Allah - Mtukufu Anasema - ***"Hakika Rehema za Allah ziko karibu na watu wema." [Al-araf: 56]***, Kisha Allah pamoja

na Msamaha Wake, na Huruma Yake, ni mkali wa kuadhibu. Mtukufu Amesema: ***"Waambie waja wangu ya kwamba Mimi ni Mwingi wa Kusamehe, na Mwingi wa Huruma. Na hakika Adhabu Yangu ni Adhabu inayoumiza kweli kweli."*** ***[Al-Hijr: 49 -50]*****.**

## Masharti ya Toba

Hakika toba ya kweli ina masharti, ambayo Wanawachuoni waliyachukua kutoka kwenye Aya na Hadithi mbali mbali, ambayo ni:

**Ya kwanza**: Kujing'oa (kuacha kabisa) dhambi kwa haraka.

**Ya pili**: Kujutia yaliyo pita.

**Ya tatu**: Kuweka azma ya kutorudia dhambi mara nyingine.

**Ya nne**: Kurejesha haki za wale alio wadhulumu, na awatake msamaha. Mtume ﷺ amesema, *"Yeyote ambaye ana chochote cha dhulma cha ndugu yake Muislam, na ajivue nacho leo leo, kabla haijafika siku ambayo hakuna Dinari wala Dirham, isipokuwa*

*mema yake na mabaya yake."* [Imepokelewa na Bukhari], lakini yule asiyeweza kurejesha haki za watu baada ya kutumia juhudi kubwa, basi Msamaha wa Allah unategemewa.

## Katika Haki:

**a) Haki za kimali**: Hii inatakiwa irejeshwe kwa mwenyewe kwa kutumia njia yeyote ile, au kujihalalishia kwake kwa kumuomba msamaha mhusika na kukubaliwa msamaha wake.

Kama hamfahamu mwenyewe, au alimtafuta hakufanikiwa kumpata, au alisahau kiasi cha mali aliyoichukua kwa huyo mtu, huyu anatakiwa akadirie hiyo haki na atoe sadaka hicho kiwango alichokikadiria.

**b) Haki za Kimwili:** Hii inatakiwa mtu atubu, nayo ni kumpa mamlaka yule mwenye haki achukue haki yake, ima kwa mali (fidia), au kisasi, au kusamehe, na kama mwenye haki hamfahamu basi anatakiwa amtolee sadaka na kumuombea dua kwa wingi.

**c) Dhulma katika kuvunja heshma za watu:** Kama vile dhulma ya kusengenya, au kumsingizia mtu zinaa, au umbea, au kuwagombanisha ndugu, huyu anatakiwa ajivue kwa yule aliyemkosea, na akitengeneze kile alichokiharibu kiasi inavyowezekana, pia kumuombea Duaa.

# Baadhi ya Aina za Toba

**1. Toba ya mtu aliyeua:**

Inawajibika kwa aliyeua kwa kukusudia kutekeleza haki tatu.

**Ya kwanza**: Haki ya Allah - Mtukufu - hii malipo yake ni toba ya kweli, kujuta juu ya hilo kosa kubwa.

**Ya pili**: Haki ya Warithi, hii malipo yake ni mtu kujisalimisha kwao, ili waweze kuchukua haki yao, kwa Kisasi, Fidia ama Msamaha.

**Ya tatu**: Haki ya mtu aliyeuwawa. Hii haiwezekani kutekelezwa hapa Duniani. Sasa kama toba ya muuaji itakuwa nzuri, na akajisalimisha kwa ndugu

wa muuliwa, basi Allah Atamsamehe na Atamlipa yule aliyeuwawa siku ya Kiyama malipo yaliyo bora zaidi kutoka kwake.

2. **Toba ya mtu aliyekula Riba:**

Hii inakuwa kwa kuacha Riba, kuazimia kutorudia tena, na kujutia matumizi ya Riba yaliyopita. Ama mali anazo miliki ambazo alizipata kwa njia ya Riba, wametofautiana Wanachuoni katika hukumu yake: Lakini anaona Ibn Taymiya, Ibn Saadiy, na Ibn Uthaymin, kwamba yafaa kwa anayemiliki mali za Riba kubaki nazo, kwa sharti awe alizipata kabla ya kutubia na wala haimlazimu kuzitoa. Lakini anatakiwa aache kupokea mali zote za riba zitazokuja baada ya toba. Dalili ya haya ni Kauli ya Allah - Mtukufu - ***"Na Amehalalisha Allah Biashara na Akaharamisha Riba, yeyote atakayejiwa na Mawaidha kutoka kwa Mola wake na akaacha (riba), yatamfaa yale yaliyopita na jambo lake lipo kwa Allah."***

# Toba ya Kweli

Ili Toba ikubalike, inatakiwa ifanywe kwa Ikhlas (kwa ajili ya Allah), hawezi kuonekana mtu ametubia, kwa kuacha kwake madhambi kwa sababu yanaharibu heshima yake ama yanamuharibia nafasi yake ya kazini.

Hawezi kuhesabika mtu ametubia kwa kule kuacha dhambi kwa sababu za kiafya, kama vile mtu akaacha zinaa kwa kuogopa maradhi, na yasiyokuwa hayo.

Hawi mwenye kutubia, aliyeacha kuiba kwa sababu hawezi, ama anamuogopa mlinzi, na mfano wa hayo.

Haitwi mtu katubia, aliyeacha pombe au madawa ya kulevya kwa sababu ya kufilisika.

Na wala haitwi mtu katubia yule anayeshindwa kufanya maasi kutokana na sababu zilizo nje ya utashi wake.

Ni lazima kwa anayetubu kuhisi ubaya wa madhambi aliyoyafanya. Hii inamaanisha toba iliyo

sahihi haiwezekani kwa mtu ambaye bado anahisi ladha ya madhambi yake, na kufurahi pale anapokumbuka madhambi yake yaliyopita, au akawa anatamani kuja kurejea tena kutenda madhambi hayo baadae.

Kama ilivyo lazima kwa mtu anayetubu, kujitakasa na mambo ya haramu yaliyopo, Mfano: ulevi, vyombo vya michezo, au picha na filamu za haramu, pia kuwaepuka marafiki waovu, ambao wanamsaidia kwenye kutenda maasi. Na hawa marafiki baadhi yao watawalaani wenzao siku ya Kiyama. Ndio ikalazimika kwa anayetubia kujiweka nao mbali, ikiwa hawezi kuwalingania na kuwafanya wawe watu wema. Na huja Shetani akapambana kwa wanaotubu kuweza kurejea kwa marafiki zao waovu, kwamba watawalingania, pamoja na kwamba wao ni dhaifu hawataweza kuwaathiri, bali hilo litakuwa ndio sababu ya yeye kurudi kwenye madhambi. Itamlazimu achague badala ya hao marafiki wabaya wengine wema watakaomsaidia katika mambo ya kheri na kumwelekeza katika mambo hayo ya kheri.

# Mambo Yanayomsaidia Mtu Kutubu

**1. Kutenda kwa Ikhlas (kufanya kwa ajili ya Allah):** Hii ndio njia yenye manufaa zaidi kwenye kuacha madhambi, atapofanya Ikhlas mja kwa ajili ya Mola wake mlezi, na akafanya toba ya kweli, Allah Atamsaidia kwenye hilo, na Atamuondoshea kila linalokuwa kikwazo kwake katika kufanya toba.

**2. Kuilazimisha nafsi:** Mwanadamu akiilazimisha nafsi yake kwenye kuacha maasi, Allah - Mtukufu - Atamsaidia: ***"Na wale wanaojitahidi kwa ajili Yetu, kwa yakini Tutawaongoza kwenye Njia Yetu, na bila shaka Allah Yu pamoja na wafanyao mema" [Ankabut: 69]***.

**3. Kuikumbuka Akhera:** Akikumbuka Mwanadamu ufupi wa Dunia, na uharaka wa kuondoka kwake, na neema zilizopo Akhera kwa wenye kumtii Allah, na ukali wa Adhabu kwa wenye kumuasi, hakika hiyo itakuwa ni kizuizi kikubwa cha kumzuia kuingia kwenye madhambi.

**4. Kujishughulisha na mambo yenye kuleta manufaa, na kujiepusha na upweke na faragha:** Faragha ndio katika sababu muhimu ya mtu kuingia katika madhambi. Mwanadamu atapojishughulisha kwa jambo lenye manufaa kwake katika Dini na dunia yake, hapo hatokuwa na fursa ya kufanya uovu.

**5. Kujiweka mbali na vishawishi na kila lenye kumkumbusha maasi:** Mwanadamu anatakiwa anajiweka na kila lenye kuamsha vishawishi vya maasi. Pia kila lenye kuamsha hisia za matamanio ya kuangalia filamu, kusikiliza nyimbo chafu, kusoma vitabu vyenye uovu, na majarida yasiyokuwa na maadili.

**6. Kusuhubiana na watu wema, na kujiweka mbali na watu waovu:** Jambo hilo linamsaidia mtu kufanya mambo ya kheri, na kumuhamasisha kuwaiga watu wema, na kujizuia na mambo ya ufisadi.

**7. Kuomba Duaa:** Hii ndio dawa yenye manufaa zaidi. Duaa ndio silaha ya Muumini, na ndio katika njia kuu ambayo inamsaidia mtu kutatuliwa shida zake. Allah - Mtukufu Amesema: ***"Na Amesema Mola wenu Mlezi, niombeni Nitawajibu." [Ghafir: 60].*** Akasema tena: ***"Muombeni Mola wenu kwa unyenyekevu na kwa siri." [Aaraaf: 55]*** Akasema tena: ***"Na waja wangu watakapokuuliza hakika Yangu, (waambie kuwa) Mimi Niko karibu nao, Naitika maombi ya mwombaji anaponiomba, basi waniitikie na waniamini, ili wapate kuongoka." [al-Baqara: 186].***

# Vitu Vinavyofuta Madhambi

Katika Huruma ya Allah Mtukufu kwa waja wake, kwamba katika baadhi ya Ibada Alizoziwajibisha kwa waja wake, huwa zinafuta madhambi madogo madogo. Na miongoni mwa ibada zinazofuta madhambi ni:

1. **Swala tano:** Mtume ﷺ amesema, *"Hivi mwaonaje! Lau mto ungepita kwenye mlango wa mmoja wenu, ikawa anaoga hapo mara tano kila siku, hivi kingebakia chochote katika uchafu wake?*" Wakasema: "Hapana ewe Mtume ﷺ." Akasema: *"Ndio kama hivyo swala tano, Allah Anafuta madhambi na makosa kupitia hizo."* [Imepokelewa na Ahlu Sunan].

2. **Swala ya Ijumaa**: Mtume ﷺ amesema, *"Atakaye tawadha na akaufanya vizuri udhu, kisha akaenda kuswali Ijumaa, akanyamaza na kusikiliza, atasamehewa madhambi yaliyopo kati ya Ijumaa hiyo na Ijumaa nyingine, na nyongeza ya masiku matatu…"* Imepokelewa na Muslim.

3. **Swaumu ya Ramadhani:** Mtume ﷺ amesema, *“Atayefunga Ramadhani kwa kumuamini Allah, na kutaraji malipo kwake, atasamehewa madhambi yake yote yaliyotangulia.”* Bukhari na Muslim.

4. **Ibada ya Hajji**: Mtume ﷺ amesema, *“Mwenye kufanya ibada ya Hijja kisha hakufanya vitendo vibaya, wala maneno machafu, atarudi akiwa amesamehewa madhambi yake kama siku aliyozaliwa.”* Bukhari na Muslim.

5. **Funga ya siku ya Arafa**: Mtume ﷺ amesema, *“Funga ya siku ya Arafa, inafuta madhambi ya mwaka uliopita na uliobaki (uliopo).”* Ameipokea Ahmad.

6. **Matatizo na Maradhi**: Mtume ﷺ amesema, “*Haimpati Muislam tabu yeyote, wala Maradhi, wala Kero, wala Huzuni, wala Maudhi, wala Majonzi, hata miba inayomchoma, isipokuwa Allah Atamfutia makosa yake.”* Bukhari na Muslim.
Mtume ﷺ akasema tena: *“Yule atakaye mtakia kheri Allah, basi Humpa mtihani.”* Ameipokea Bukhari.

7. **Istighfar (kuomba Msamaha kwa Allah)**: Hakika jambo kubwa ambalo Allah Anafuta madhambi kupitia hilo ni *Istighfar*. Allah - Mtukufu Amesema - ***"Allah Hakuwa Mwenye Kuwaadhibu, ilihali wanataka Istighfar (wanaomba msamaha)" [Anfal: 33]***, Mtume ﷺ amesema, *"Hongera kwa yule ambaye atakuta kwenye Kitabu chake Istighfari (kuomba msamaha) nyingi."* Ameipokea Ibn Majah, na Baihaqy.

# Maswali na Majibu:

**Swali**: Nataka kutubu lakini Madhambi yangu ni mengi sana, na wala sifahamu! Hivi Allah Atanisamehe yote niliyoyafanya kwenye miaka yote iliyopita?

**Jibu**: Allah Anasema: ***"Sema Enyi waja wangu mliojidhulumu nafsi zenu! Msikate tamaa na Rehema za Allah, bila shaka Allah Husamehe dhambi zote, hakika Yeye ni Mwingi wa Kusamehe, (na) Mwingi wa Kurehemu." [Az-Zumar: 53].***

Allah Amesema tena katika *Hadithil-Qudsiy*: **"Ewe Mwanadamu! Hakika utakaponiomba na kunitaraji Mimi Nitakusamehe madhambi uliyonayo yote wala Sitojali. Ewe Mwanadamu! Iwapo madhambi yako yatafikia umbali wa mbingu, kisha ukaniomba msamaha, Nitakusamehe na wala Sitojali. Ewe Mwanadamu! Hakika wewe ukinijia Mimi na makosa yenye ujazo wa Ardhi, kisha ukanijia bila kunishirikisha na**

**chochote kile, Nitakujia na Msamaha kwenye ujazo huo." [Imepokelewa na Imam Tirmidhiy].**

Bali Ukarimu wa Allah kwa waja wake ni mkubwa zaidi kuliko hayo. Hakika mwenye kuifanya toba yake kuwa ya kweli, basi Allah Humbadilishia makosa yake yote yaliyotangulia kuwa mema. Kama Allah Alivyosema: ***"Isipokuwa waliotubu wakaamini na kufanya matendo mema, hao ndio Allah Atawabadilishia maovu yao kuwa mema" [Furqan: 70].***

**Swali**: Nataka kutubu lakini marafiki wabaya hawatoniacha, na mimi nahisi unyonge (sina uwezo), nifanyeje?

**Jibu**: Ni lazima kusubiri na kuendelea na toba, na huko ni kutahiniwa, ili aweze kupambanuka yule mkweli kwenye toba yake na asiyekuwa mkweli. Lakini pia lazima kuchukua tahadhari ya kutowatii, Allah - Mtukufu - Anasema: ***"Basi subiri (ewe Muhammad) hakika ahadi ya Allah ni kweli, na wala wasikubabaishe wale wasiokuwa na yakini" [Ar-Rum: 60].*** Mtu anatakiwa atambue kuwa

marafiki waovu watatumia njia nyingi tofauti ili wamrejeshe kwao, kisha baada ya kujua ukweli wake, na nguvu zake kwenye haki, watamuacha.

**Swali**: Nataka kutubu lakini marafiki zangu wa zamani wananitisha kuwa watanifedhehesha, kwa matendo niliyoyafanya, na kwamba wao wana picha na vielelezo, na mimi naogopea kuchafuliwa utu wangu, nifanyeje?

**Jibu**: Kwanza kabisa pambana na marafiki wa Shetani, na tambua kuwa vitimbi vya Shetani ni dhaifu.

Kisha tambua ukiwakubalia, watapata vithibitisho zaidi, hapo utakuwa umepata hasara mwanzo mwisho, lakini mtegemee Allah. Sema: **“*Toshelezo langu ni Allah, nae ni mbora wa kutegemewa.*”**

Mtume ﷺ alikuwa akiwaogopa watu, husema: *“Ewe Allah hakika sisi tunakuweka katika shingo zao, na tunajilinda Kwako na shari zao.”* [Ameipokea Ahmad, na Abuu Daud].

Kiusahihi msimamo huu ni mgumu, lakini Allah Yuko pamoja na wachamungu na wala hawadhalilishi. Chukua hiki kisa ambacho kina ushahidi bora juu ya Msaada wa Allah kwa wanaomcha.

“Ni Swahaba: Murthid Bin Abii Murthid, alikuwa akiwatorosha wale wanyonge, katika Waislam, kutoka Makka kwenda Madina. Na alikuwepo Makka Mwanamke muovu, anaitwa ‘Anaaq’ na alikuwa ni rafiki yake. Huyu (Swahaba) aliahidiana na mtu ampeleke Madina, anasema Murthid: “Nikaenda mpaka nikafika kwenye kivuli cha ukuta, kwenye usiku wa mbalamwezi, akaja Anaaq akaniona, aliponikaribia akanifahamu kisha akasema: ‘Twende tukalale pamoja usiku huu wa leo.’ Nikamjibu: ‘Ewe Anaaq! Allah Ameharamisha Zinaa.” Anaaq akasema: ‘Enyi watu! Huyu anawachukua (anawatorosha) Mateka wenu. Wakanifuata wananikimbiza watu wanane, mpaka nikafika kwenye pango nikaingia. Wakaja mpaka wakasimama katibu na kichwani kwangu, Allah Akawapa upofu wa kutoniona. Kisha wakarudi, nami nikarudi kwa yule rafiki yangu nikamchukua na kumpeleka

Madina." Ndio kama hivi Allah Huwasaidia na Kuwahami waumini na wenye kutubu.

Kisha kama yatakuwa wazi yale unayoyaogopea, na ikahitajika kuyaweka wazi zaidi, basi weka wazi msimamo wako kwa wengine, na waambie! 'Ni kweli nilikuwa nafanya madhambi lakini kwa sasa nimetubu.' Tukumbuke ya kwamba fedheha ya kweli, ni ile itayokuwa mbele ya Allah siku ya Qiyama, na mbele ya Viumbe wote, Malaika, Majini na Watu.

**Swali**: Mimi nafanya madhambi na ninatubu, kisha nafsi yangu inanishinda, narejea tena kwenye dhambi! Je toba yangu ya kwanza inabatilika, kisha yakabaki madhambi yale ya mwanzo na haya mengine?

**Jibu**: Anayetubia dhambi, Allah Anakubali toba yake, na akirejea tena kufanya dhambi kwa mara nyingine, atakuwa kama vile amefanya Maasi mapya, atatakiwa atubu tena, na toba yake ya kwanza ni sahihi.

**Swali**: Je! Inasihi kufanya toba kwa dhambi fulani ilihali naendelea kufanya dhambi nyingine?

**Jibu**: Itaswihi toba kutokana na dhambi fulani, hata kama atakuwa anang'ang'ania kufanya dhambi nyingine, kwa sharti isiwe ile anayoifanyia toba. Mfano: Mtu akifanya toba kwa ajili ya Riba, na hakutubu kwa ajili ya kunywa pombe, toba yake kwenye Riba iko sahihi, lakini akitubia kunywa pombe kisha akawa anatumia Madawa ya kulevya, au ametubia kutokana na kuzini na mwanamke fulani kisha akawa anang'ang'ania kuzini na mwanamke mwingine, toba hii sio sahihi.

**Swali**: Nimeacha baadhi ya Faradhi katika masiku yaliyopita, zikiwemo, Swala, Funga, na Zaka, nifanye nini?

**Jibu**: Ama Swala sio wajibu kuilipa, lakini badala yake inatakiwa ifanywe toba ya kweli na kudumisha kuswali, kufanya Istighfari (kuomba msamaha) kwa wingi, ili Allah Aweze Kukusamehe.

Ama aliyeacha Swaumu, kama alikuwa Muislam atalazimika kulipa tangu alipoacha, na pia

kuwajibika kulisha masikini (fidia) kwa hesabu ya siku alizoacha. Ama yule aliyeacha kutoa Zaka atalazimika atoe.

**Swali**: Nimeiba Mali za watu, na nimetubu kwa makosa hayo, lakini sizifahamu anuani zao.

**Jibu**: Utalazimika kuwatafuta kiasi cha uwezekano, ukiwapata wape mali zao ulizochukua kwao. Kama mwenye mali amekufa wakabidhi warithi wake. Na kama usipowaona, pamoja na kutumia juhudi kubwa ya kuwatafuta, basi toa sadaka kwa niaba yao. Nuia thawabu ziende kwao. Kama watakuwa Makafiri, basi Allah Atawalipa hapahapa Duniani na wala hatowapa chochote kesho Akhera.

**Swali**: Nimefanya kosa la Zinaa! Vipi nitatubu? Na kama mwanamke atapata ujauzito huyu mtoto ni wa kwangu?

**Jibu**: Kama zinaa ilifanyika kwa ridhaa ya mwanamke na kukubali, haiwajibiki kwako isipokuwa toba tu, na mtoto hawi wako, na wala haiwajibiki kwako matumizi yake. Kwa kuwa ni

mtoto wa zinaa, na mtoto kama huyu huwa anakutanishwa na nasaba ya mama yake tu.

Wala haijuzu kwa mtu aliyetubia zinaa kumuoa mwanamke huyu kwa lengo la kusitiri lile tukio la aibu. Ama akitubu mwanamume na mwanamke pia akatubu na zikawa toba za kweli, hakutakuwa na ubaya wa kumuoa, baada ya kuyakinisha kuwa hana ujauzito kwenye mfuko wake wa uzazi.

Kama zinaa ilikuwa ya kubaka ama kumlazimisha mwanamke, katika hali hii itawajibika kwa mwanamume kutoa mahari ya mfano wake. Ikiwa ni kama mbadala wa madhara aliyomsababishia, na atubie toba ya kweli, pamoja na kumsimashia Haddi (Adhabu), kama jambo likifikishwa kwenye utawala.

**Swali**: Nimeolewa na mtu mwema na nilifanya mambo ambayo hayamridhishi Allah kabla ya kuolewa, nini nifanye?

**Jibu**: Unawajibika kufanya toba ya kweli, na wala huwajibiki kumuambia mumeo yale uliyoyafanya.

**Swali**: Mambo gani yanawajibika kwa mwenye kutubia kosa la kulawiti?

**Jibu**: Ni wajibu kwa mtenda na mtendewa kufanya toba kubwa, kwani yeye anatambua yale Aliyoyafanya Allah kwa watu wa Nabii Lutwi, kutokana na ubaya wa makosa yao. Hakika Allah Alifanya yafuatayo:

a) Aliwapofoa macho yao wakakawa vipofu.

b) Aliwatumia sauti kali ikawa sababu ya kifo chao.

c) Aliing'oa miji yao na Kuiinua mbinguni kisha Kuigeuza.

d) Aliwateremshia mvua ya mawe ya udongo wa kuchoma, yaliyopangiliwa, akawaangamiza wote.

Kwa sababu hiyo, ndio Mtume ﷺ akasema: *"Mkiwakuta watu wanafanya matendo ya watu wa Lutwi, basi muueni mtenda na mtendewa." [Ameipokea Abuu Daud, At-Tirmidhy na Ibn Majah]*.

Itamlazimu kwa mwenye kufanya matendo haya toba ya kweli, na kumuomba msamaha Allah, kwa wingi.

Mwisho: Kumbuka ewe ndugu yangu kipenzi, Allah Ana Huruma zaidi kuliko mama kwa mwanawe. Mtu atayefanya toba ya kweli Allah Anamkubalia toba yake. Mlango wa toba uko wazi wala haufungwi.

Rehema za Allah zimuendee Muhammad, na jamaa zake na Masahaba wake wote.

Shukrani zote ni za Allah Ambaye kwa Neema Zake ndio hutimia mambo mema.

# Yaliyomo

**Utangulizi** ........................................................3

**Fadhila za Toba.** ...............................................3

**Masharti ya Toba** ............................................12

**Baadhi ya Aina za Toba** ....................................14

**Toba ya Kweli** ..................................................16

**Mambo Yanayomsaidia Mtu Kutubu** .................18

**Vitu Vinavyofuta Madhambi** ..............................21

**Maswali na Majibu:** ..........................................24